

## 17-Al-Qalqalah (Kugonga)

قلْلَةٌ Maana yake kilugha ni kutikisika, kusogea, kutokuwa na utulivu.

Katika hukmu ya Tajwiyd, ni mgongano wa kutetema unaosababishwa na herufi maalum za qalqalah zinapokuwa na sukuwn<sup>1</sup>, aidha iwe ya asili au ya kuzuka kwa ajili ya kusimama. Herufi za qalqalah zimekusanyika katika ibara: قُطْبُ جَدًّ

Qalqalah inagawanyika katika daraja mbili

### 1. القُلْلَةُ الْكُبِرَى Al-Qalqalatul-Kubraa -Qalqalah Kubwa

Inapokuwa herufi ya qalqalah mwisho wa neno lenye kusimamiwa.

### 2. القُلْلَةُ الصُّغْرَى - Al-Qalqalatus-Sughraa - Qalqalah Ndogo

Inapokuwa herufi ya qalqalah katikati ya neno au mwisho wa neno lakini si neno lenye kusimamiwa.

الْقُلْلَةُ الْكُبِرَى Al-Qalqalatul-kubraa (Qalqalah kubwa)	الْقُلْلَةُ الصُّغْرَى Al-Qalqalatus-sughraa (Qalqalah ndogo)	Herufi
وَتَصَدَّقَ	لَوْقَعَتْهَا	ق
تُشَطِّطُ	مَطَّلَعٍ	ط
يُعَقِّبُ	عَبْدِهِ	ب
فَآخْرُجَ	أَجْمَعُونَ	ج
وَسَخَنَدُ	فَادْعُوا	د

<sup>1</sup>Imeshaelezwa kwa kifupi katika mlango wa 'Swiffah za Herufi'